

WARAKA WA TATU WA YOHANA

¹ Mimi mzee nakuandikia wewe Gayo, rafiki yangu, ninayekupenda kweli.

² Mpenzi wangu, nakutakia mafanikio mema ya kila aina; nakutakia afya njema ya mwili kama ulivyo nayo rohoni.

³ Nimefurahi sana ndugu kadhaa walipofika hapa, wakaiambia juu ya uaminifu wako kuhusu ukweli; naam, wewe unaishi daima katika ukweli.

⁴ Hakuna kitu kinachonifurahisha zaidi kuliko kusikia kwamba watoto wangu wanaishi katika ukweli.

⁵ Mpenzi wangu, wewe ni mwaminifu kila mara unapowahudumia ndugu, hata kama ni wageni.

⁶ Ndugu hao wamelieleza kanisa hapa habari za upendo wako. Tafadhalii uwasaide waendelee na safari yao kwa namna itakayompendeza Mungu,

⁷ Maana wanaanza safari yao katika utumishi wa Kristo bila kupokea msaada wowote kutoka kwa watu wasioamini.

⁸ Basi, sisi tunapaswa kuwasaidia watu hawa, ili nasi tupate kushiriki katika kazi yao kwa ajili ya ukweli.

⁹ Niliandika barua fupi kwa hilo kanisa; lakini Diotrefe, ambaye hupenda kuwa kiongozi wao, hataki kabisa kunisikiliza.

¹⁰ Basi, nitakapokuja nitayafichua mambo yote anayofanya, maneno mabaya anayotutolea na uongo anaosema juu yetu. Isitoshe, ye ye

hukataa kuwakaribisha hao ndugu walio safarini, na hata huwazuia watu wengine wanaotaka kuwakaribisha, na hujaribu kuwafukuzia nje ya kanisa.

¹¹ Mpenzi wangu, usifuate mfano mbaya, bali mfano mwema. Kila atendaye mema ni wa Mungu; lakini anayetenda mabaya hajapata kumwona Mungu.

¹² Kila mtu anamsifu Demetrio; naam, ukweli wenyewe unamsifu. Nasi pia tunatoa ushahidi wetu juu yake, nawe wajua kwamba tunachosema ni kweli.

¹³ Ninayo bado mengi ya kukwambia, lakini sipendi kuyaandika kwa kalamu na wino.

¹⁴ Natumaini kukuona karibuni na hapo tutazungumza ana kwa ana. (G1-15) Nakutakia amani. Rafiki zako wanakusalimu. Wasalimu rafiki zetu wote kila mmoja binafsi.

Biblia Takatifu
Portions of the New Testament in the Swahili
Language of Kenya, Mozambique, Somalia, and
Tanzania, translation by Dr. Johann Ludvig Krapf
completed in 1850

Public Domain

Language: Kiswahili (Swahili)

Dialect: Kimvita

Translation by: Dr. Johann Ludvig Krapf

2014-08-25

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 18 Apr 2025 from source files
dated 31 Aug 2023

62071dc0-70e6-5b86-b569-c1b45e7771bd